# JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

## MAMLAKA YA UDHIBITI WA NAFAKA NA MAZAO MCHANGANYIKO
## BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA
## TUME YA MAENDELEO YA USHIRIKA TANZANIA SOKO LA BIDHAA TANZANIA

# MWONGOZO WA BIASHARA KWA MAZAO YA DENGU, MBAAZI, SOYA, UFUTA, CHOROKO, NJUGUMAWE NA KUNDE KWA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA NA MINADA YA KIDIJITALI

**Toleo la Tano (5) - Mwaka 2026**

## UTANGULIZI

Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania , Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Bidhaa Tanzania kwa pamoja wana jukumu la kuhakikisha kuwa hali ya masoko na kipato cha mkulima kinaimarika kupitia uzalishaji wa mazao yenye ubora na yaliyoongezwa thamani ili kukidhi mahitaji ya soko. Vilevile, kuweka mifumo imara ya masoko ili kumpatia mkulima soko la uhakika na bei yenye tija kwa mazao yake.

Ili kuhakikisha upatikanaji wa soko la uhakika na uimara wa bei, taasisi hizi zimekusudia kuwepo kwa Mfumo imara wa uzalishaji, ukusanyaji, utunzaji, uuzaji , malipo ya mazao yanayozalishwa kwa wakati na kumwezesha mnunuzi kupata mazao yenye ubora unaostahili kwa mujibu wa Sheria zinazosimamia uzalishaji na uuzaji wa mazao.

Kutambua umuhimu wa mfumo katika kuimarisha masoko ya bidhaa za wakulima na kupunguza changamoto zinazotokana na mauzo ya mazao, mwongozo huu umeandaliwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko, Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania, Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na Soko la Bidhaa Tanzania kwa lengo la uuzaji wa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde utakaotekelezwa katika mikoa yote ya Tanzania Bara inayozalisha mazao hayo.

Mwongozo huu unabainisha mifumo ya uuzaji wa mazao inayopaswa kutumika kwa wakati mmoja katika msimu wa kilimo kulingana na matakwa ya muuzaji. Mifumo hii inampatia mnunuzi na muuzaji fursa ya kusogezewa soko la uhakika kwa kuzingatia ushindani wa bei, uharaka wa malipo, ubora na wingi wa mazao kulingana na mahitaji ya soko.

Mwongozo huu utatambulika kama ***"Mwongozo wa Biashara kwa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde Toleo la 4-2026 Uliotolewa chini ya Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC), Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) na Soko la Bidhaa Tanzania (TMX)"***

Mwongozo huu unazingatia Sheria ya Usalama wa Chakula Sura 249 katika Kifungu cha 4(2)(e), (i), Sheria ya Ushirika Sura 211 Kifungu cha 142(k) na Kanuni zake za Mwaka 2015 Kanuni ya 81(1)(a),(b) pamoja na Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura ya 339 Kifungu cha 6(1)(l) na Kanuni zake za Mwaka 2016 pamoja na Sheria ya Soko la Bidhaa Sura 445.

## TAFSIRI YA MANENO YALIYOTUMIKA

Katika mwongozo huu, maneno yafuatayo yanatafsiriwa kama ifuatavyo:-

**Chama cha Msingi:** *Maana yake ni Chama cha Msingi cha Ushirika kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Sura 211*

**Chama Kikuu:** *Maana yake ni Chama Kikuu cha Ushirika kilichosajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Sura 211.*

**"Ghala la Mnada:** *Maana yake ni ghala lililokidhi sifa na vigezo kwa ajili ya kukusanya* Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde *za wakulima yatakayouzwa kupitia mfumo wa Stakabadhi za Ghala.*

**Mazao bila Daraja (BD):** *Ni mazao ambayo hayajapewa daraja lakini yamezingatia viwango vya usafi, unyevu, rangi na umbo*

**Mfumo wa Stakabadhi za Ghala:** *Maana yake ni mfumo wa soko ambapo mazao huhifadhiwa katika Ghala Kuu lililopatiwa Leseni na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na kutolewa stakabadhi ikionesha kiasi, ubora na daraja la mazao kwa lengo la kusubiri kuuzwa.*

**Mweka Mali:** *Mkulima/mwakilishi au wakala wa mkulima wake aliyerasimishwa kuweka mali zake ghalani.*

**Mwendesha ghala/Mtunza Ghala:** *Kampuni iliyosajiliwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kujishughulisha na biashara ya kuendesha ghala kwa lengo la kupokea na kuhifadhi mazao jamii ya kunde kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura ya 339*

**Akaunti ya Pamoja:** *Maana yake ni akaunti iliyofunguliwa benki na Chama Kikuu cha Ushirika kwa ajili ya kudhibiti mtiririko wa fedha za malipo ya mazao kutoka kwa wanunuzi kwenda akaunti za vyama vya msingi ikiwa ni pamoja na wakulima na walipwaji wengine kwa kuzingatia mjengeko wa bei.*

**Ghala la Chama cha Msingi:** *Maana yake ni kituo cha kukusanyia* Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde *za wakulima kwa ajili ya kuzipeleka katika ghala kuu la mnada*

**Katalogi ya Mauzo:** *Maana yake ni kijarida cha mauzo ya mazao (sales catalogue) kinachoonesha aina ya zao, idadi katika kilo, ubora, loti na ghala la mnada mazao husika yalipohifadhiwa.*

**Lot:** *Maana yake ni fungu la mazao yaliyopo katika ghala la mnada zinazosubiri kuuzwa kwenye mnada*

**Mhakiki wa Ubora:** *Maana yake ni mtaalam aliyefuzu mafunzo ya uhakiki ubora wa mazao na kupata cheti kutoka mamlaka ya zao husika na kuajiriwa na Mwendesha Ghala kwa ajili ya kuhakiki ubora wa mazao yanayoingia katika Ghala Kuu*

**Mkaguzi wa Ubora:** *Maana yake ni mtaalam wa kukagua ubora wa mazao yaliyopo kwenye ghala, gari, shamba, kiwanda na mahali pengine popote ambapo panapohusika na* Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde

**Mnunuzi:** *Maana yake ni mfanyabiashara (kampuni au mtu binafsi) aliyesajiliwa na Mamlaka (COPRA) na ataruhusiwa kununua Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kupitia minada ya kidijitali inayoendeshwa na TMX. Kutakua na usajili wa aina mbili za wanunuzi kama ifuatavyo:*

***Mnunuzi wa soko la ndani** – huyu ni mnunuzi anayenunua kwa ajili ya **mauzo ya ndani ya nchi tu** na ataruhusiwa kununua hadi Tani 30 ndani ya msimu mmoja kwa kuweka punguzo ya dhamana ya Kinga ya Tsh. 5,000,000 tu.*

***Mnunuzi mkubwa na/au msafirishaji nje ya nchi (exporter)** – Huyu ni mnunuzi atakayenunua kuanzia Tani 30 na kuendelea kwenye minada na kuweka dhamana ya kinga kama ilivyoainishwa kwenye Jedwali Na. 1 kwenye mwongozo huu.*

**Msafirishaji:** *Maana yake ni kampuni inayohusika kusafirisha mazao kwa mujibu wa taratibu zilizopo*

**PDN (Produce Dispatch Note):** *Maana yake ni hati ya kusafirisha mazao ndani ya nchi.*

**Sheria:** *Maana yake ni sheria ya Vyama vya Ushirika Sura 211,* Sheria ya Usalama wa Chakula Sura 249, *Sheria ya Stakabadhi za Ghala sura 339 pamoja na Sheria ya Soko la Bidhaa Sura 445.*

| | |
|---|---|
| *TBS (Tanzania Bureau of Standards):* | *Maana yake ni Shirika la Viwango Tanzania.* |
| *TRA (Tanzania Revenue Authority):* | *Maana yake ni Mamlaka ya Mapato Tanzania.* |
| *WMA (Weights and Measures Authority):* | *Maana yake ni Wakala wa Vipimo Tanzani* |

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0. UTARATIBU WA MAUZO YA MAZAO KUPITIA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA

Kwa mujibu wa Vifungu vya 4(1), na 4(2)(e), (f), (i), (j) vya Sheria ya Usalama wa Chakula ya Mwaka 1991 na Marekebisho ya Mwaka 2023 ambavyo vimetoa mamlaka kwa COPRA kufanya shughuli za usimamizi wa kwenye mnyororo mzima wa thamani ikiwemo mfumo wa masoko ya nafaka na mazao mchanganyiko ikielekeza urasimishaji wa wadau na mali (premises) kwa kufanya usajili, ukusanyaji wa taarifa, utoaji vibali, kutengeneza mfumo wa usimamizi pamoja na usimamizi wa shughuli zote zenye manufaa kwenye nafaka na mazao mchanganyiko ikiwemo mazao kuuzwa katika mfumo rasmi bila kuathiri Kifungu cha 83 cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura 339 na Marekebisho ya 2016 utaratibu ulioainishwa utahusu waweka mali wanaouza mazao yao kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala.

### 1.1. Ukusanyaji wa Mazao ya Mkulima/Mweka mali

Katika kutekeleza mfumo wa mauzo waweka mali (wakulima) katika vituo vya kukusanyia vilivyopo chini ya chama cha msingi, isipokuwa katika mikoa yenye wakusanyaji mazao/wakulima wakubwa kama ilivyoainishwa katika **Kiambatisho Na. 1**, watatakiwa kuzingatia masuala yafuatayo: -

i. Mkulima/mweka mali wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kwa ajili ya kuuza atapeleka katika vituo vya ukusanyaji vinavyoratibiwa na Chama cha Msingi akiwa amezipanga kwenye madaraja yanayotambulika kwa mujibu wa mwongozo huu ambayo yametajwa **Kipengele** 1.2.2 (ii) (A) na (B);

ii. Chama cha Ushirika cha Msingi kitahakikisha kuwa mzani unaotumika kupimia Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde ghalani umekaguliwa na Wakala wa Vipimo Tanzania (WMA) kabla ya kuanza kwa msimu;

iii. Chama cha Ushirika cha Msingi kitapokea Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kutoka kwa wakulima na kuhakiki ubora; kabla ya kuzipima uzito na kuziweka katika viroba vipya;

iv. Chama cha Ushirika cha Msingi kitampatia mkulima stakabadhi ya mapokezi ya zao lake ghalani ikiwa na taarifa muhimu za mkulima kama vile jina kamili, tarehe ya kupima, idadi ya vifungashio, uzito, nambari ya akaunti ya benki au simu inayopokea fedha na namba ya simu;

v. Chama cha Ushirika cha Msingi kitatoa taarifa ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde iliyopokolewa kila baada ya siku mbili kwa COPRA ikiwa na majina ya wakulima, nambari za stakabadhi za ghala walizokatiwa pamoja na kiasi kilichopokelewa.

vi. Chama cha Ushirika cha Msingi kwa kushirikiana na taasisi simamizi za mfumo kitahakikisha kuwa wakulima/waweka mali wanapata mafunzo ya msingi ya usimamizi wa ubora ikiwemo uanikaji/ukaushaji, usafi, kupima unyevu na ufungashaji;

vii. Chama cha Ushirika cha Msingi kitahakikisha kuwa uzito halisi wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde ni kilo hamsini ( 50 ) tu kwa kila kifungashio kabla ya kupeleka kwenye ghala la mnada;

viii. Chama cha Ushirika cha Msingi kitaandika namba ya utambulisho wa nembo ya chama kikuu husika, namba ya usajili wa chama cha ushirika cha msingi kwa kutumia rangi za maandishi zilizochaguliwa na chama kikuu husika.

ix. Chama cha Ushirika cha Msingi kitapeleka Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde ya wakulima/waweka mali kwenye ghala la mnada lililosajiliwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kwa ajili ya mauzo;

x. Chama cha Msingi kitasafirisha Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde ya wakulima/waweka mali kwenda ghala la mnada kwa kutumia PDN ya Chama cha Ushirika cha Msingi ikiambatana na **fomu ya orodha ya wakulima/waweka mali iliyojazwa kikamilifu ikionyesha wamiliki husika ikiwa katika nakala nne**; nakala ya kwanza ipelekwe kwa Afisa Ushirika, Msimamizi wa ghala husika, nakala ya pili Chama Kikuu husika, nakala ya tatu ipelekwe kwa Mtunza Ghala la mnada na nakala ya nne ibaki katika Chama cha Msingi husika;

xi. Gharama za kusafirishia Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde zitakuwa sawa na gharama zilizopangwa katika mjengeko wa bei uliopo katika mwongozo huu.

## 1.2. Ukusanyaji na Usimamizi wa Ghala Kuu

Utaratibu ufuatao utatumika katika Ghala Kuu zilizopewa leseni chini ya Kifungu cha 16 cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala.

**1.2.1. Upatikanaji wa Mwendesha Ghala katika mauzo ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde.**

a. Waendesha Ghala watapaswa kuomba leseni Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kwa kuzingatia Kifungu cha 16 cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala, Kanuni na Miongozo;

b. Chama Kikuu kitatangaza zabuni, kuchambua na kupitisha kampuni ya mwendesha Ghala mwenye leseni ya Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kwa kuzingatia Kifungu cha 16 cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala, Kanuni na Miongozo;

c. Mwendesha ghala atakuwa analipwa asilimia 55% ya malipo yake kwa kila mnada, na kiasi kitakachobaki atalipwa kwa mkupuo mwisho wa msimu. Fedha hizi zitahifadhiwa na vyama vikuu vya ushirika.

**1.2.2. Wajibu wa Mwendesha Ghala katika Kupokea Mazao**

i. Kupokea na kutoa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde yakiwa katika hali ya usafi na yaliyokauka vema.

ii. Kusafisha mazao na pale inapowezekana, kwa kutumia mtambo maalum wa usafishaji, ili mazao ya dengu, mbaazi, soya, ufuta na choroko yakidhi viwango vya ubora vya Shirika la Viwango Tanzania TBS yakiwa hayana uchafu au mbegu za mazao mengine kama ifuatavyo:

**A : Daraja la Kwanza (GRADE 1), Daraja la Pili (GRADE 2)** na **Daraja la Tatu (GRADE 3)** kwa mujibu wa Viwango kama ifuatavyo : -

| **Na.** | **Aina ya Zao** | **Kiwango kisizidi** |
|---|---|---|
| 1 | Dengu | TZS 1667:2014(1st Ed)/EAS 754:2013 |
| 2 | Mbaazi | TZS 1084:2014/EAS 756:2013 |
| 3 | Soya | TZS 1083:2018/EAS 762:2017 |
| 4 | Choroko | TZS 1666:2014 |
| 5 | Ufuta | TZS 741:2018 |
| 6 | Njugumawe | ISO 9001 |
| 7 | Kunde | TZS 1668:2014(E) |

**B: Mazao Bila Daraja (BD)**

i. Yatapokelewa ghalani kwa makubaliano kati ya Mwendesha Ghala na Mweka Mali baada ya vigezo vifuatavyo kuhakikiwa: -

a. Rangi ya zao;
b. Kiwango cha unyevu;
c. Kiwango cha uchafu *(foreign matter);*
d. Kiwango cha mbegu zilizooza;
e. Kiwango cha mchanganyiko wa mbegu nyingine.
f. Umbo

ii. Viwango vya Unyevu wa mazao yatakavyopokelewa ghalani utakuwa kama ifuatavyo.

| Na. | Aina ya Zao | Kiwango Kisizidi |
|---|---|---|
| 1 | Dengu | 8.50% (w/w) |
| 2 | Mbaazi | 8.50% (w/w) |
| 3 | Soya | 8.50% (w/w) |
| 4 | Choroko | 11.50%(w/w) |
| 5 | Ufuta | 7.50% (w/w) |
| 6 | Njugumawe | 7.0-8.0%(w/w) |
| 7 | Kunde | 10.0% (w/w) |
| **Na.** | **Aina ya Zao** | **Kiwango Kisizidi** |
| 1 | Dengu | 8.50% (w/w) |
| 2 | Mbaazi | 8.50% (w/w) |
| 3 | Soya | 8.50% (w/w) |
| 4 | Choroko | 11.50%(w/w) |
| 5 | Ufuta | 7.50% (w/w) |
| 6 | Njugumawe | 7.0-8.0%(w/w) |
| 7 | Kunde | 10.0% (w/w) |

iii. Kufungasha mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kwa kutumia mifuko maalum itakayotolewa na Chama Kikuu cha Ushirika yenye kukidhi vigezo vya viwango vya TBS kwa kutumia mtambo maalum.

iv. Kuhakikisha mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde yanayopokelewa yanaambatana na orodha ya wakulima/waweka mali husika;

v. Kuandaa Cheti cha Ubora kwa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kwa kila stakabadhi ya ghala itakayotolewa ghalani,cheti hiki kitahakikiwa na Mamlaka ya udhibiti wa nafaka na mazao mchanganyiko COPRA ;

vi. Kuwa na vifaa muhimu vya kupima vigezo vya ubora ambavyo vitajumuisha,

a. Chekeche ya maabara *(Laboratory Analysis Sieve)/mashine ya kusafishia*
b. Kipima unyevu *(Moisture Meter)* cha zao la Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;
c. Mizani ya maabara iliyothibitishwa na Wakala wa Vipimo;
d. Bambo ya kuchukulia sampuli kutoka kwenye vifungashio;
e. Vijiko vya maabara vinavyotosheleza mahitaji ya upimaji wa sampuli

f. Bakuli za kupimia sampuli;
g. Ubao maalum wa sampuli;
h. Kisu/kikatio cha maabara;

vii. Kuhakikisha kuwa vifungashio vyote vina jina kamili la Mweka Mali;

viii. Kuhakikisha kuwa taarifa ya kiasi cha mzigo kilichosafishwa ikiwa imeorodhesha kiasi cha uchafu uliotoka inaandaliwa na kuthibitishwa na Chama cha Ushirika, Afisa Ushirika na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko;

ix. Kuhifadhi Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kwa utaratibu wa kiboharia wa kutunza mazao ghalani na kwa kuzingatia madaraja ya ubora;

x. Kuhakikisha upangaji unawezesha mazao yaliyoingia kwanza ndiyo yatakayo toka kwanza (FIFO) katika ghala;

xi. Endapo nafasi ya ghala inaruhusu, Mwendesha Ghala anaweza kupanga bidhaa kwa kila mweka mali kuwa na fungu lake (stake);

xii. Kuhakikisha kila kifungashio kitakachotumika katika kujaza mazao yaliyomwagika ghalani kinazingatia utaratibu wa Kipengele (vii) hapo juu;

xiii. Kupokea kidijitali kutoka TMX na kuhakiki Hati ya Ankara ya Mauzo (Invoice), Agizo la Kutoa Mazao Ghalani (Release Warrant), na Stakabadhi ya Ghala husika kabla ya kuruhusu kutoa ghalani;

xiv. Kuhakiki idadi ya vifungashio vya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde vinavyotolewa ghalani kulingana na Stakabadhi husika;

xv. Kupima uzito wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde wakati wa kuingia ghalani;

xvi. Kupima unyevu wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde wakati wa kutoa ghalani;

xvii. Kutoa kwa Mnunuzi Hati ya Toleo la Stakabadhi **{Warehouse Receipt Issue Note (WRIN)}** kwa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde inayotolewa ghalani;

xviii. Kutoa taarifa ya mapokezi **(Fomu Namba 5)** na ya utoaji **(Fomu Namba 6)** kila siku kwa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde itakayopokelewa au kutolewa ghalani kwenye kanzidata ya Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala na Mamlaka;

xix. Kwa kuzingatia masharti yaliyopo katika Sheria ya Stakabadhi za ghala, kujaza **Fomu Namba 7** na kuwasilisha taarifa ndani ya **siku saba (7)** tangu kubainika kwa tatizo husika. Fomu itakayochelewa zaidi ya muda tajwa itachukuliwa kuwa ni batili.

xx. Vifungashio vitakavyotumika ni vipya tu na vifungashio ambavyo mkulima ataletea mazao yake katika ghala/vituo vya ukusanyaji atarejeshewa mara baada ya mazao yake kupokelewa.

### 1.2.3. Viwango vya Utendaji katika Ghala Kuu Kwenye Mfumo wa Stakabadhi Za Ghala Mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde

i. Vifungashio vyote vitakavyotumika vitakuwa vipya na vinavyokidhi viwango vya kimataifa **ISO 23560:2015** na kuidhinishwa na Shirika la Viwango Tanzania ambapo; uzito wa kila kifungashio ni **gram 100**, urefu wa nje **milimita 965** na upana wa nje **milimita 560**;

ii. Uzito wa zao katika kila kifungashio ghalani ni **kilogram hamsini (50) tu**. Iwapo vifungashio vitakuwa havina uzito wa **kilogram 50** za Zao, ni wajibu wa Mweka Mali kufananisha vifungashio vyote kwa lengo la kupata uzito wa **kilogram hamsini (50) tu** kwa kila kifungashio;

iii. Kiwango cha juu cha urefu wa steki ya vifungashio vya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde hautakiwi kuzidi mita tatu (3m) kutoka kwenye chaga; aidha, urefu hautakiwi kuzidi sehemu ya chini ya dirisha la kuingizia hewa (vent) hata kama mita tatu (3m) hazijafikiwa

iv. Nyaraka za ndani ambazo ni lazima zitumike katika ghala lililosajiliwa na Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala ni:-

***Wakati wa Kupokea mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde Ghalani: -***

a. Orodha ya majina ya waweka mali waliowasilisha Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde husika kwa kila stakabadhi;
b. Hati ya Mweka Mali ya kukabidhi mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde ghalani –"Produce Delivery Note" (PDN);
c. Hati ya kuhesabu idadi ya vifungashio – "Tally Sheet" (TS);
d. Hati ya kupima uzito – "Weight Note" (WN);
e. Hati ya kupokea Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde ghalani – "Goods Received Note" (GRN).

***Wakati wa Kutoa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde ghalani: -***

a. Nakala ya Ankara ya mauzo ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde – "Sales Invoice";
b. Hati ya Toleo la Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kutoka benki au kwa muuzaji –"Release Order (Warrant)";
c. Agizo la kuchukua Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde ghalani kutoka kwa Mnunuzi –"Dispatch Order";Kidijitali
d. Hati ya kuhesabu idadi ya vifungashio – "Tally Sheet" (TS);
e. Cheti cha Ubora – "Quality Certificate" (QC);
f. Hati ya kupima uzito – "Weight Note" (WN);
g. Hati ya kutoa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde Ghalani – "Warehouse ReceiptIssue Note" (WRIN)

***Nyaraka Nyingine;***

a. Rejesta katika Idara mbali mbali;
b. Bin Card katika kila steki iliyopo katika ghala la kuhifadhi Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde ;
c. Kitabu cha Ukaguzi wa Taarifa za Ghala za Kila Siku;
d. Hati ya mazao yaliyokataliwa itasainiwa na Afisa Ushirika, Afisa wa COPRA, Meneja Mkuu wa Chama cha Ushirika na Mwendesha Ghala.

v. Upungufu wa idadi ya vifungashio vya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde katika Stakabadhi yoyote hauruhusiwi na iwapo ikitokea Mwendesha Ghala atalipa kwa thamani ya bei ya mnada pamoja na adhabu ya **asilimia 5 iwapo kiasi cha mazao kimepungua na atalipa adhabu ya asilimia 2 pekee ya mifuko iliyokosekana iwapo hakuna kiasi cha mzigo kilichopungua.**

vi. Stakabadhi yoyote itakayobakia bila kuwa na mazao ghalani ni ukiukwaji wa viwango vya utendaji wa Mwendesha Ghala husika. Stakabadhi hii italipwa kwa bei ya mnada pamoja na adhabu ya asilimia 20. Mwendesha Ghala atatoa taarifa ya upotevu wa mazao ghalani katika kituo cha Polisi cha karibu ndani ya saa 24 tangu kubainika kwa tukio nakuwasilisha taarifa hiyo Bodi (WRRB) na Mamlaka (COPRA).

vii. Muda wa kuhifadhi mazao ghalani bila malipo ya ziada (adhabu) kwa mnunuzi ni **siku kumi (10)** tangu kutolewa kwa Ankara ya Malipo (siku hizi hazitajumuisha Jumamosi na Jumapili);

viii. Baada ya **siku ya kumi (10)** tangu kutolewa kwa Ankara ya Malipo na **WRRB kujiridhisha kuwa mzigo haujatolewa**, Mnunuzi atalazimika kulipia gharama ya ziada ya kuhifadhi mazao ya **Shilingi 10.0/=** kwa kilo kwa siku, kwa **siku kumi na moja (11)** zinazofuata. Gharama hizi zitalipwa moja kwa moja kwenye akaunti ya Mwendesha Ghala.

ix. Ifikapo siku ya **ishirini na moja ( 21 )** endapo mnunuzi hajaanza au hajamaliza kutoa mzigo wake ghalani na baada ya kuthibitishwa na WRRB, **Basi mnunuzi huyo hataruhusiwa kushiriki minada inayofuata.**

x. Mwendesha Ghala anaweza kutoa taarifa ya maandishi na/au Ilani Namba 2 kwa mnunuzi akimwagiza kutoa bidhaa ghalani wakati wowote **kabla ya siku ya 21** tangu kutolewa kwa Ankara ya Malipo. Pia, Mwendesha Ghala atawasilisha taarifa Bodi (WRRB) kwa hatua za kutoa taarifa kwa wadau akiwemo COPRA kuhusu utekelezaji wa **Kifungu cha (ix)** endapo Mwendesha Ghala atataja kuwa kuchelewa kwa mnunuzi kunaathiri shughuli za uhifadhi ghalani mwake.

xi. Mnunuzi atahesabiwa ameshindwa kabisa kutoa mazao ghalani baada ya **siku ishirini na moja (21)** tangu siku ya mauzo;

xii. Mazao yatakayoshindikana kutolewa na mnunuzi **Kipengele (xi)**, yatataifishwa na Serikali chini ya uratibu wa COPRA kwa kushirikiana na Serikali ya Wilaya husika na yatauzwa kwenye mnada utakaopangwa. Fedha zitakazopatikana, pamoja na mambo mengine, itafidia gharama za uendeshaji kwa pande husika;

xiii. Muda wa kuhifadhi dengu, njugumawe, kunde, mbaazi, soya, ufuta na choroko kwa Mweka Mali (Muuzaji) ni **siku 30** tangu tarehe ya kuandikwa Stakabadhi husika. Iwapo kutakuwepo na tatizo la soko, Mweka Mali au Wakala wake atatakiwa kuomba ruhusa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kuongezewa muda wa ziada. Uamuzi wa kuongezewa muda na gharama zake utatolewa na Bodi;

xiv. Mazao ambayo yatafikishwa ghalani yakiwa na uchafu, unyevu mkubwa, idadi ya vifungashio isiyolandana na uzito na utofauti wa kumbukumbu hazitapokelewa na Mwendesha Ghala.

xv. Mnunuzi ahakikishe ubora wa mazao **kabla** ya kuyatoa ghalani baada ya kufanya malipo na iwapo kuna kasoro ambayo haijatolewa ufumbuzi na mwendesha ghala atatakiwa atoe taarifa kwa taratibu zilizotolewa na mwongozo huu kwenda WRRB kwa usuluhishi. Iwapo mnunuzi atakua hajaridhika na maamuzi ya WRRB na **hayuko tayari kuchukua mzigo** anatakiwa kukata rufaa kwa Mamlaka (COPRA) ili kupata usuluhishi.

xvi. Muda wa Mwendesha Ghala kupokea au kutoa bidhaa ghalani ni kati ya **saa moja kamili asubuhi (1:00)** hadi saa kumi na **mbili kamili jioni (12:00)**; taarifa zote za ghala zinapaswa kukamilika kupakiwa kwenye kanzidata ndani ya muda huo.

## 1.3. Mauzo ya dengu, njugumawe, kunde, mbaazi, soya, ufuta, na choroko Kupitia Soko la Bidhaa Tanzania

Kwa mujibu wa **Kifungu cha 70A (1)** cha Sheria ya Stakabadhi za Ghala,

mauzo ya bidhaa katika Mfumo wa Stakabadhi za Ghala yatafanyika kupitia Soko la Bidhaa *(Commodity Exchange)* linaloendeshwa na Tanzania Merchantile Exchange (TMX);

**1.3.1. Kabla ya Mnada**

i. Wanunuzi kujisajili kupitia COPRA na kisha kujaza fomu TMX ya kuridhia kushiriki minada kwa njia ya kielektroniki.

ii. Wanunuzi wataweka Kinga ya Dhamana kwenye akaunti maalum ya Soko la bidhaa Tanzania (TMX) ambayo husimamia minada ya kidijitali kwa utaratibu ulioainishwa katika jedwali Na 1 hapo chini. Kinga hii ya dhamana inaweza kutumika kwa zao zaidi ya moja na utaratibu wa uwekaji, utoaji na matumizi ya dhamana hii, utatolewa na TMX.

**Jedwali Na. 1**

| Na. | KIASI KWA TANI | GHARAMA YA KINGA YA DHAMANA |
|---|---|---|
| 1 | **Tani 30 hadi 50** | **30,000,000** |
| 2 | **Tani 51 na kuendelea** | **100,000,000** |

iii. Kiwango cha Kinga ya Dhamana kwa wanunuzi wenye usajili wa kununua mazao kwa ajili ya soko la ndani ya nchi kitakuwa TZS milioni 5 na wanunuzi hawa wataruhusiwa kununua hadi Tani 30 ya zao husika kwa. msimu wa mauzo. Wanunuzi wengine watatumia utaratibu ulioainishwa katika kipengele 1.3.1 (ii) hapo juu.

iv. Mnunuzi aliyekamilisha hatua ya usajili na Kinga ya Dhamana anaingizwa kwenye Mfumo wa Mauzo wa Kielektroniki wa TMX;

v. Wakulima/waweka mali wanakusanya mazao kupitia vituo vya ukusanyaji vinavyoratibiwa na Vyama vya Ushirika vya Msingi (AMCOS) kisha kupelekwa ghala kuu. Usafirishaji wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kutoka AMCOS kuelekea ghala kuu utakuwa kuanzia saa 12:00 asubuhi hadi saa 12:00 jioni;

vi. Taarifa ya kiasi kilichopokelewa ghala kuu itaingizwa kwenye kanzidata ya WRRB na Nakala ya taarifa kwa COPRA;

vii. Hati ya mauzo *(Sales catalogue)* itaandaliwa na kutumwa kwa wadau mbalimbali siku moja kabla ya siku ya mnada;

viii. Chama Kikuu cha Ushirika kitaandaa hati ya mauzo *(Sales Catalogue)* kwa kushirikiana na COPRA, WRRB na TMX kisha kuituma kwa wadau mbalimbali;

ix. Taarifa za hati ya mauzo *(Sales Catalogue)* zitaingizwa kwenye Mfumo wa Mauzo wa TMX na mafungu *(Lots)* kupangwa kwa kuzingatia vituo vya ukusanyaji (AMCOS) au uwingi wa mazao kufuatia upangaji kwenye ghala kuu na pia madaraja;

x. Mfumo wa Mauzo wa Kielektroniki utafunguliwa kwa ajili ya wanunuzi wenye kupenda kuweka bei ya ununuzi kabla ya mnada kuanza ( *PreBid)* ndani

ya saa moja kabla ya mnada kuanza. Bei hii itaonekana kwa mnunuzi tu mpaka pale mfumo utakapofunguliwa kwa wanunuzi kuanza kushindana.

xi. Chama Kikuu kama mwakilishi wa waweka mali atatakiwa kukubaliana na COPRA na TMX juu ya bei anzia ya kuuzia mazao yatakayouzwa katika mnada husika saa moja kabla ya mnada kufanyika.

### 1.3.2. Wakati wa Mnada

i. Kabla ya mnada mweka mali atahitajika kukubaliana na TMX na COPRA juu ya bei anzia katika mnada husika na kukiri kuwa bei itakayopatikana juu ya bei anzia itahesabika kuwa amekubali kuuza mazao yake;

ii. Iwapo bei anzia haitakubaliwa na waweka mali kupitia Chama Kikuu, basi mnada husika hautafanyika;

iii. Minada itafanyika kwa njia ya kielektroniki kwa wanunuzi kuweza kushiriki popote walipo kwenye eneo lenye mtandao;

iv. Endapo kuna wanunuzi waliofanya Pre-Bid, bei ya juu itakayopatikana ndio bei itakayoanzia kwenye fungu *( Lot)* husika kwa wanunuzi kuanza kushindana;

v. Wanunuzi watashindana kununua kwa fungu *(Lot)* (fungu moja ikiwa ni kiasi chote cha aina ya mazao kilichowasilishwa na AMCOS husika au mgawanyo kufuatia uwingi wa mazao kwenye ghala);

### 1.3.3. Baada ya Mnada

i. Chama Kikuu cha Ushirika baada ya kupata idhini ya wakulima, kitaridhia au kukataa bei zilizopatikana kupitia TMX kwa njia ya mfumo ,wa mauzo wa kidijitali ndani ya saa moja baada ya mnada kuisha;

ii. TMX kwa kushirikiana na Chama kikuu cha Ushirika watatoa taarifa ya mnada na kuwasilisha kwa wadau;

iii. TMX kwa kushirikiana Chama Kikuu cha Ushirika wataandaa, kuhakiki na kuwasilisha kwa mnunuzi aliyeshinda Hati ya Madai (Sales invoice);

iv. Mnunuzi aliyeshinda atafanya malipo ndani ya siku tatu (masaa 72) za kazi tokea kupokea hati ya madai (Sales invoice);

v. Malipo yote yatalipwa kwenda Chama Kikuu cha Ushirika husika, ambacho kitafanya mgawanyo wa malipo kwa taasisi na wadau husika ndani ya masaa 72.

vi. TMX kwa kushirikiana na Chama Kikuu cha Ushirika watandaa Release Order na kuiwasilisha kwa wanunuzi;

vii. Mnunuzi atachukua mazao aliyonunua baada ya kujiridhisha na alichokilipia.

### 1.3.4. Utoaji wa Taarifa za Mauzo

i. Kwa Mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula ya Mwaka 1991 Sura 249 na Marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ya Mwaka 2009 katika Kifungu cha 4(b) Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko itatoa bei ya kuanzia kwenye minada kwa kushirikiana

na Soko la Bidhaa Tanzania;

ii. Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko itatoa taarifa za mwenendo wa soko la Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kila wiki kipindi cha msimu wa ununuzi kupitia vyombo vya habari ikiwemo mitandao ya kijamii na tovuti za taasisi husika.

iii. Kila Chama cha Msingi kitabandika taarifa za mauzo ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde za wakulima wake kwenye mbao za matangazo za chama chake.

## 1.4. Usafirishaji wa dengu, mbaazi, soya, ufuta na choroko

i. Mnunuzi atasafirisha Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kwa kutumia PDN inayotolewa na Chama husika pamoja na nyaraka zote halali za ununuzi wa mazao kutoka katika Halmashauri husika;

ii. Uongozi wa Halmashauri kwa kushirikiana na kamati za ulinzi na usalama pamoja na kamati ya usimamizi wa mfumo watahakikisha kuwa mazao yote yanayosafirishwa ni yale yaliyonunuliwa kwenye mnada.

## 1.5. KAMATI ZA USIMAMIZI WA MFUMO WA STAKABADHI ZA GHALA (WRS)

Ili kuongeza ufanisi katika usimamizi wa shughuli za mfumo, Kifungu cha 6(3) cha Sheria ya Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala inazipa Mamlaka za Serikali za Mikoa na Wilaya kuweka kamati za usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika maeneo yao. Ambapo Kifungu cha 6(4) cha Sheria ya Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala kinaeleza Katibu Tawala Mkoa kuwa Mwenyekiti katika ngazi ya Mkoa na Mkurugenzi Mtendaji kuwa Mwenyekiti katika ngazi ya Wilaya. Muundo wa kamati hizo utakuwa kama ilivyotajwa katika Jedwali la Tano katika Kanuni za Stakabadhi za Ghala za 2016. Majukumu ya kamati hizo ni kama ifuatavyo: -

i. Kuhakikisha waweka mali wanalipwa kwa kiasi na ubora waliowasilisha;
ii. Wadau wengine kulipwa kwa mujibu wa huduma walizotoa;
iii. Kuhamasisha matumizi ya Mfumo katika maeneo yao;
iv. Kutolea ufafanuzi masuala mbalimbali yanayojitokeza katika maeneo yao;
v. Kutoa taarifa kwa Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za ghala kila mwezi, roboya mwaka na mwaka;
vi. Kushauri Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za ghala juu ya masuala mbalimbaliya Mfumo;
vii. Kutekeleza majukumu mengine kama itakavyoelekezwa na Bodi ya Usimamiziwa Stakabadhi za ghala au umuhimu utakavyojitokeza.

## SEHEMU YA PILI

**2.0. MAJUKUMU YA TAASISI/ MAMLAKA MBALIMBALI KUPITIA MFUMO**

**2.1. Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA)**

a. Kusajili wakulima, maghala, wasafishaji, wanunuzi.

b. Kufuatilia mwenendo wa bei ya mazao husika kwenye soko la dunia na ndani na kuwashauri wadau;

c. COPRA kutoa bei elekezi kwa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde pale itakapohitajika kutokana na uhalisia wa soko;

d. Msimamizi wa taratibu zote kwenye utekelezaji wa mwongozo ;

e. Kutangaza kuanza na kufungwa kwa msimu wa mauzo.

f. Kukusanya, kuchambua na kusambaza taarifa na takwimu zinazohusiana na Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kwa mujibu wa Kifungu cha 4(2)(c) cha Sheria ya Usalama wa Chakula ya mwaka 1991 Sura 249 na Marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ya Mwaka 2023;

g. Kuandaa na kusimamia viwango *(standards)* katika mnyororo wa thamani wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;

h. Kulinganisha taarifa zilizoko katika ghala kuu vile vile kulinganisha taarifa kutoka kwa wakulima na zilizopo chama kikuu kwa stakabadhi husika;

i. Kuandaa Miongozo ya Uchakataji, uhifadhi, masoko na usafirishaji nje ya nchi kwa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;

j. Kufanya ukaguzi wa maeneo na vituo vyote vya mauzo ya mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;

k. Kusimamia na kudhibiti ukusanyaji, usafirishaji, uhifadhi, mauzo, ununuzi, masoko, usindikaji/uchakataji, usambazaji, usafirishaji nje ya nchi, utekekezaji *(Disposal),* na ugavi/ upatikanaji *(Supply)* wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;

l. Kutoa vibali vya uingizaji ndani na utoaji nje ya nchi. Aidha, vibali vya kusafirisha nje ya nchi mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde vitatolewa kwa **mnunuzi mkubwa na/au msafirishaji atakayetoa nyaraka za kuthibitisha ununuzi kupitia minada ya kidijitali (TMX) kwa kuzingatia taratibu za Maboresho ya Mwongozo Toleo 4-2026** au nyaraka ya kuthibitisha mizigo inayopitia kutoka nchi za jirani (on-transit);

m. Kutoa usajili kwa wanunuzi wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;

n. Kukagua mashamba, nafaka, mali, ghala zenye mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde.

o. Kutathmini, kusimamia na kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma ikiwemo wasafishaji wa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde.

p. Majukumu ya kusimamia na kuhamasisha kilimo na ubora wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde.

**2.2. Tume ya Maendeleo ya Ushirika (TCDC)**

a. Kuhakikisha vyama vya ushirika vina uwezo wa kufanya biashara ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde na kutunza kumbukumbu zote za mauzo;
b. Kuhakikisha vyama vya ushirika vinakuwa na maghala ya awali /vituo vya ukusanyaji na vfungashio vya kutosha kuhifadhia Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;
c. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara wakati wa msimu kwenye vyama vya ushirika;
d. Kuhamasisha Vyama vya Ushirika kulipa wakulima kupitia njia ya akaunti ya benki ausimu kwa wakati;
e. Kuhakikisha Vyama vya Ushirika vinatumia mifumo ya kidigitali wakati wa utekelezajiwa biashara ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;
f. Kusimamia utekelezaji wa mwongozo kwa mujibu wa sheria ya ushirika Na.6 yamwaka 2013.

**2.3. Vyama Vikuu vya Ushirika**

a. Chama Kikuu cha Ushirika kitaandaa hati ya mauzo *(Sales Catalogue)* kwa kushirikiana na COPRA na TMX;
b. Kupitia Mfumo wa TMX, kuwasilisha maamuzi ya wakulima juu ya kuridhia au kukataabei iliyopatikana sokoni;
c. Kwa kushirikana na TMX Kutuma Hati ya Madai kwa wanunuzi walioshinda;
d. Kwa kushirikiana na TMX,Kutoa hati ya utoaji mazao yaliyouzwa (*Release Order)* kwa wanunuzi waliolipa;
e. Kuwasilisha taarifa ya mauzo kwenye AMCOS na wakulima mara baada yakupokea kutoka TMX;
f. Kuandaa na kusambaza shajala kwa ajili ya ukusanyaji Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde katika vyama vya msingi;
g. Kusimamia shughuli za uendeshwaji wa biashara ya mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kupitia AMCOS;
h. Kusimamia utekelezaji wa majukumu ya wasafirishaji ambao wameingia mikataba na vyama vya ushirika;
i. Kufanya malipo ya fedha za wakulima kwa mauzo ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde kwa kushirikiana na maafisa ushirika wa wilaya husika, viongozi wa menejiment za AMCOS husika;
j. Kuhamasisha wakulima kupitia AMCOS kufungua akaunti zitakazotumiwa kupokea malipo ya mauzo ya mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;
k. Kupanga ratiba za minada na kuiwasilisha COPRA ili itangazwe kwa Umma. Iwapo kuna mabadiliko yoyote ya ratiba za minada yawasilishwe COPRA; na
l. Kutunza kwa usahihi takwimu za ununuzi wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta,

Choroko, Njugumawe na Kunde kutoka kwa wakulima na kutoa taarifa kwa Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania (TCDC) pamoja na wadau wengine wa usimamizi pindi zitakapohitajika;

### 2.4. Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB)

a. Kwa kushirikiana na COPRA kufanya usaili wa waendesha maghala kabla ya kutoa leseni.
b. Kutoa leseni kwa Waendesha Ghala;
c. Kutoa taarifa ya Waendesha Ghala waliopewa leseni;
d. Kusimamia Waendesha Ghala kuhakikisha bidhaa zinazopokelewa ghala kuu zinazingatia Sheria, Kanuni na Miongozo iliyopo;
e. Kuwezesha upatikanaji wa takwimu za Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde zilizopokelewa ghalani;
f. Kufanya ukaguzi wa mara kwa mara kwenye ghala zinazoendesha biashara ya mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;
g. Kutatua changamoto na migogoro inayohusisha waendesha ghala, waweka mali na wanunuzi.

### 2.5. Soko la Bidhaa Tanzania (TMX)

a. Kwa kushirikiana na COPRA kuingiza wanunuzi kwenye mfumo wa kielektroniki wa TMX;
b. Kwa kushirikiana na COPRA, kuhakiki na kuwajulisha wanunuzi juu ya Hali ya Kinga bei zilizowekwa;
c. Kuhakiki hati ya mauzo *(Sales Catalogue)* na kuituma kwa wadau mbalimbali;
*d.* Kufungua Mfumo wa Mauzo wa Kielektroniki kwa ajili ya wanunuzi kufanya *Pre-Bid;*
e. Kutuma Hati ya Madai Kielektoniki kwa wanunuzi walioshinda kwa kushirikiana na Vyama vikuu vya Ushirika;
f. Kutoa hati ya utoaji mazao yaliyouzwa (*Release Order)* kwa wanunuzi waliolipa; kwa kushirikiana na Vyama vikuu vya ushirika.
g. Kutoa taarifa ya mnada husika kwa wadau;
h. Msimamizi mkuu wa Mfumo wa Mauzo wa Kielektroniki;
i. Kwa kushirikiana na COPRA pamoja na Vyama Vikuu vya Ushirika katika kuandaa na kutangaza tarehe za minada;
j. Kuwasilisha hati ya Mauzo kwa njia ya kielektroniki kwa wanunuzi na wadau husika mapema kabla ya minada;
k. Kushirikiana na wadau wengine kutatua migogoro inayotokana na malipo au miamala baada ya mauzo;
l. Kwa kushirikiana na COPRA, kutafuta na kutangaza taarifa za mwenendo wa bei za soko kwa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde ;

**2.6. Halmashauri/Wilaya**

a. Kuhamasisha kilimo cha Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde na kusimamia ubora katika maeneo yao;
b. Kutangaza bei za mazao zinazopatikana katika minada kwa wakulima na jamii kwa ujumla kupitia nyenzo mbali mbali katika Halmashauri husika.
c. Kuandaa mfumo wa kudhibiti na kuzuia ununuzi nje ya mfumo rasmi wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;
d. Kuundaa, kusimamia na kugharamia vikosi kazi katika Halmashauri ili kutekeleza mfumo wa kudhibiti ununuzi nje ya mfumo rasmi wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde pamoja na kutatua changamoto zote zinazojitokeza katika maeneo yao;
e. Kufuatilia mwenendo wa zao kuanzia uzalishaji, ukusanyaji, mauzo, malipo na usafarishaji wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde katika maeneo yao;
f. Kuundaa kamati za usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika maeneo yao.

**2.7. Sekratarieti za Mkoa**

a. Kuhamasisha kilimo cha Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde na kusimamia ubora katika maeneo yao ya mkoa;
b. Kuandaa na kuratibu vikao vya wadau wa mazao ya Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde;
c. Kufuatilia mwenendo wa mazao kuanzia uzalishaji, ukusanyaji, mauzo, malipo nausafarishaji wa Dengu, Mbaazi, Soya, Ufuta, Choroko, Njugumawe na Kunde katika maeneo yao;
d. Kuanzisha na kusimamia kamati za usimamizi wa Mfumo wa Stakabadhi za Ghala katika ngazi ya mkoa.

**2.8. Shirika la Ukaguzi na Usimamizi wa Vyama vya Ushirika (COASCO)**

Kupitia fedha ya ukaguzi inayokusanywa katika kupitia utekelezaji wa Mwongozo, COASCO itatekeleza masuala yafuatayo:

a. Kukagua utendaji katika vyama vikuu vya ushirika na vyama vya msingi wakati wa utekelezaji wa Mwongozo
b. Kukagua malipo kutoka Vyama vikuu vya Ushirika kwenda kwa wakulima wakati wa utekelezaji wa Mwongozo
c. Kukagua uwepo wa nyaraka mbali mbali za utendaji katika vyama vya ushirika kulingana na Mwongozo huu
d. Kukagua taarifa za mwishoni mwa msimu za utekelezaji kwa vyama vya ushirika
e. Kutoa taarifa ya ukaguzi na utekelezaji kwa Kamati tendaji ya utekelezaji wa Mwongozo

## SEHEMU YA TATU

**3.0. MENGINEYO**

**3.1. Kilimo Cha Mkataba**

Kilimo cha mkataba kitafanyika baada ya kuwa mkataba husika umesajiliwa na COPRA kufuatia taratibu zilizowekwa katika usajili wa Kilimo cha Mkataba. COPRA baada ya kusajili kilimo cha mkataba husika atatakiwa kutoa taarifa kwenye Mamlaka ya Mkoa na Halmashauri ya Wilaya kwa ajili ya uangalizi na utekeleza wa mikataba ya kilimo kwa ufanisi. .

**3.2. Usuluhishi wa Migogoro**

Mgogoro wa aina yeyote baina ya upande mmoja na mwingine utatatuliwa kwa mujibu wa Kifungu Na. 6 – (1) (b) cha Sheria ya Usalama wa Chakula Sura 249 na Marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ya Mwaka 2023, Kanuni ya 83 ya Kanuni ya vyama vya ushirika ya mwaka 2015.

**3.3. Gharama Mbalimbali**

Kwa mujibu wa Sheria ya Usalama wa Chakula Sura 249 na Marekebisho yaliyofanywa na Sheria ya Nafaka na Mazao Mchanganyiko ya Mwaka 2023, na uhalisia wa gharama, COPRA itazibainisha na kuziorodhesha gharama mbali mbali katika mwongozo huu kwa kukidhi mahitaji yafuatayo: -

i. Gharama ya Usimamizi wa Vyama Vya Ushirika
ii. Dhamana ya Utunzaji Mazao Ghalani;
iii. Vifungashio;
iv. Usafirishaji;
v. Ukaguzi;
vi. Gharama za uendeshaji mifumo ya Minada
vii. Utunzaji ghala;
viii. Gharama ya Usimamizi na Maendeleo ya zao;
ix. Gharama ya Usimamizi Mkoa;
x. Gharama ya Usimamizi Wilaya na
xi. Gharama ya kusafisha Mazao (**Hizi gharama zitalipwa moja kwa moja kwa watoa huduma ya usafishaji ambao watakua wamepewa usajili na Leseni na Mamlaka – COPRA. Gharama zitalipwa na mnunuzi kabla ya kuchukua mzigo ghalani –** *gharama hii italipwa katika maghala yenye miundombinu ya usafishaji pekee kama itakavyokuwa imeainishwa katika hati ya mauzo ya ghala husika*).

**NB**:

- *Tozo nyingine zote za maendeleo ngazi ya Mkoa na Halmashauri ambazo zipo nje na mwongozo huu, zitatolewa na wakulima kufuatia makubaliano yatakayofanyika na wana ushirika kupitia mikutano mikuu ya ushirika. Tozo hizi zitapitishwa kwenye mkutano wa wadau na kuidhinishwa na Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao mchanganyiko (COPRA);*
- *CESS itatozwa kwa kuzingatia Sheria.*

**Jedwali Na. 2.** Mjengeko wa Tozo kwa mazao ya Mikunde (Dengu, Mbaazi, Soya, Choroko, Njugumawe na Kunde);

| Na. | Aina ya Tozo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Gharama za Usimamizi za Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika | 60 |
| 2. | Mtunza Ghala | 37.5 |
| 3. | Ukaguzi | 2 |
| 4. | Dhamana ya Utunzaji Mazao Ghalani | 3.5 |
| 5. | Usafirishaji | 50 |
| 6. | Gharama za usimamizi wa mauzo | 5 |
| 7. | Usimamizi Mkoa | 2 |
| 8. | Usimamizi Wilaya | 2 |
| 9. | Vifungashio | 20 |
| 10. | Maendeleo ya zao | 30 |
| **Jumla ya tozo** | | **212 + 3% CESS** |

**Jedwali Na. 3.** Mjengeko wa Tozo kwa zao la Ufuta;

| Na. | Aina ya tozo | Kiasi |
|---|---|---|
| 1. | Gharama za Usimamizi za Uendeshaji wa Vyama vya Ushirika | 100 |
| 2. | Mtunza Ghala | 37.5 |
| 3. | Ukaguzi | 2 |
| 4. | Dhamana ya Utunzaji Mazao Ghalani | 3.5 |
| 5. | Usafirishaji | 50 |
| 6. | Gharama za usimamizi wa mauzo | 5 |
| 7. | Usimamizi Mkoa | 2 |
| 8. | Usimamizi Wilaya | 2 |
| 9. | Vifungashio | 20 |
| 10. | Maendeleo ya zao | 30 |
| **Jumla ya tozo** | | **252 + 3% CESS** |

**Jedwali Na. 4.** Mjengeko wa Tozo baada ya msimu kufungwa ndani ya mkoa wa uzalishaji;

| **Na.** | **Aina ya tozo** | **Kiasi** | |
|---|---|---|---|
| | | **Mikunde** | **Ufuta** |
| 1. | Maendeleo ya Ushirika | 42 | 47 |
| 2. | Maendeleo ya usimamizi stakabadhi za Ghala | 20 | 25 |
| 3. | Maendeleo za usimamizi wa mauzo | 20 | 25 |
| 4. | Usimamizi Mkoa | 30 | 40 |
| 5. | Usimamizi Wilaya | 50 | 60 |
| 6. | Maendeleo ya zao | 50 | 55 |
| **Jumla ya tozo** | | **212 + 3% CESS** | **252 + 3% CESS** |

**Jedwali Na. 5.** Mjengeko wa Tozo baada ya msimu kufungwa nje ya mkoa wa uzalishaji;

| **Na.** | **Aina ya tozo** | **Kiasi** | |
|---|---|---|---|
| | | **Mikunde** | **Ufuta** |
| 1. | Maendeleo ya Ushirika | 100 | 100 |
| 2 | Maendeleo ya usimamizi stakabadhi za Ghala | 100 | 100 |
| 3. | Maendeleo ya usimamizi wa mauzo | 100 | 100 |
| 4. | Maendeleo ya zao | 200 | 200 |
| **Jumla ya tozo** | | **500** | **500** |

### 3.4. Kutolewa kwa Mwongozo

| | |
|---|---|
| ........................ | ........................ |
| Irene M. Mlola | Dkt. Benson O.Ndiege |
| Mkurugenzi Mkuu | **Mrajis wa Vyama Vya Ushirika** |
| **Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko** | **Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania** |

| | |
|---|---|
| ........................ | ........................ |
| Godfrey Malekano | Asangye N. Bangu |
| **Afisa Mtendaji Mkuu** | **Mkurugenzi Mtendaji** |
| **Soko la Bidhaa Tanzania** | **Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala** |

**Tarehe ya kutolewa kwa mwongozo huu.................................**